# HUNIONGOZA MWOKOZI

He Leadeth Me, o Blessed Thought

*Author*
*Joseph Henry Gilmore*




1. Huniongoza Mwokozi, ndipo nami hufurahi, Niendapo pote napo, ataniongoza papo

***Huongoza hunishika, Kwa mkono, wa hakika,***
***Nitaandamana naye, Kristu aniongozaye***

2. Pengine ni mashakani, nami pengine rahani, Ni radhi ijayo yote, yupo nami siku zote

3. Mkono akinishika, kamwe sitanung'unika, Atakachoniletea, ni tayari kupokea

4. Ikiisha kazi chini, ntakwenda huko mbinguni, Nako nitamtukuza, Kristo aliyeongoza

*Umenakiliwa na Martin Munywoki*